JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# MAGAZETINI WIKI HII

Mji wa Serikali, Mtumba S.L.P. 315, DODOMA. Simu: +255 26 2310021 Barua pepe: km@sheria.go.tz




*PRESIDENT Samia Suluhu Hassan addresses Judges and other delegates at the Law Day climax in Dodoma, yesterday. From right is Chief Justice Prof Ibrahim Juma, Principal Judge of the High Court, Mustapher Siyani and Constitutional and Legal Affairs Minister, Dr*

**Dailynews, 02/02/2023, Uk 1**

# Jaji: Wananchi hawataki kumaliza kesi kwa usuluhishi

**Habari Leo, 02/02/2023, Uk 1**

**Na Fadhili Abdallah, Kigoma**

WANANCHI wengi katika Mkoa wa Kigoma hawataki kumaliza kesi kwa usuluhishi na wanataka mashauri yaishie mahakamani, imefahamika.

Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Kigoma, Lameck Mlacha alisema hayo jana wakati wa kilele cha wiki ya sheria kuashiria kuanza kwa mwaka mpya wa mahakama.

Jaji Mlacha alisema mwaka jana, mashauri 5,366 yalifunguliwa kwenye mahakama za Mkoa wa Kigoma ikiwemo Mahakama Kuu lakini ni mashauri 256 yaliyomalizika kwa njia ya usuluhishi sawa na asilimia 4.8 ya mashauri hayo.

Alitaja sababu za kukwama kwa mashauri kwa njia ya usuluhishi kuwa ni pamoja na kukosekana kwa utayari baina ya watu wanaohusika na shauri husika kusuluhishwa.

Jaji Mlacha alitaja sababu nyingine ni baadhi ya mawakili kutokuwa tayari kuendesha mashauri kwa njia ya usuluhishi kutokana na maslahi binafsi ya kifedha na kukosekana kwa elimu ya usuluhishi kwa wananchi.

Hata hivyo, alisema idara ya mahakama mkoani Kigoma imejiwekea mkakati kuhakikisha wanakabili changamoto hiyo kwa kutoa elimu na kuhamasisha wadau wote wa haki kushughulikia mashauri kwa njia ya usuluhishi na kueleza faida zake kwa jamii.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye alisema utatuzi wa mashauri kwa njia ya usuluhishi ni muhimu katika kukabiliana na muda, gharama lakini kurudisha amani kwa jamii.

Andengenye ametoa mwito kwa wananchi na wadau wote wanaosimamia masuala ya kupata haki kutumia fursa ya kushughulikia mashauri yao kwa njia ya usuluhishi kutokana na faida zake.

Mwanasheria wa kujitegemea, Daniel Rumenyela alisema mashauri mengi mkoani humo yanaanzia kwenye usuluhishi lakini inakwama na wengi kuona hukumu ndiyo njia pekee ya kupata haki zao.

Rumenyela alisema mashauri mengi yaliyopo yanahusiana na migogoro ya ardhi na kesi za madai na kwa nafasi zao wamekuwa wakijitahidi kuomba wahusika wazungumze na kumaliza kwa njia ya usuluhishi lakini inafika mahali usuluhishi unashindikana.

# Jaji Mkuu aagiza kesi za madai zianzie usuluhishi

Na Anastazia Anyimike, Dodoma

MAHAKAMA imependekeza kuwa iwe lazima kesi zote za madai zianze ngazi ya usuluhishi kabla ya kusajiliwa katika mahakama ili kupunguza mlundikano wa kesi na kuvutia wawekezaji.

Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Juma alisema hayo Dodoma jana wakati wa kilele cha Wiki ya Sheria.

"Itahakikisha utoaji wa haki kwa haraka, wakati, kuruhusu usiri na utatuzi wa kirafiki, urahisi wa kubadili taratibu na kupata watatuzi wenye utaalamu wa masuala ya migogoro," alisema Profesa Juma.

Alisema pamoja na sheria kutoa mwanya wa upatanishi na usuluhishi, watu wengi wanachagua kuiruka hatua hiyo na kuchagua kufungua kesi mahakamani.

Profesa Juma alisema kesi za madai zinazowasilishwa mahakamani huchukua kati ya miaka mitatu hadi 10 wakati kwa njia ya usuluhishi huchukua takribani siku 30 na mwombaji halipi chochote.

Alisema pia wamehakikisha sheria zinazotoa fursa ya usuluhishi na zimepatiwa nguvu ili kukidhi mahitaji na kuongeza ufanisi.

"Wengi wao hawajui faida katika usuluhishi huo. Kesi zikiwa mahakamani, ile dhamana inashikiliwa hadi kesi imalizike.

"Kama kesi inachukua miaka kumi, ina maana mtaji wako unashikiliwa kusubiri shauri lipitie ngazi mbalimbali. Kwenye usuluhishi, hilo halipo na hakuna gharama zozote, kwa sababu serikali inagharamia," alisema Profesa Juma.

Alitaja baadhi ya mashauri ambayo yanapaswa kupitia katika ngazi ya usuluhishi kuwa ni ardhi, kodi, masuala ya fedha, ndoa, madai na migogoro ya kazi.

Aidha, Profesa Juma alishauri mashirika ya kidini ambayo yako katika migogoro kuwasilisha masuala kwenye taasisi na mabaraza chini ya mwavuli wao na si mahakamani.

Awali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk Eliezer Feleshi alisema wameanzisha mchakato wa marekebisho ya sheria ili iwe lazima kwa kesi zote za madai kufunguliwa kwa njia ya upatanishi na usuluhishi.

Dk Feleshi alisema ni kwa njia ya usuluhishi hakutakuwa na ucheleweshaji wa haki kwa kuwa kupitia mahakama kuna mambo mengi ya kiufundi ya kujadiliwa jambo ambalo linafanya kesi kuchukua muda mrefu.

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Profesa Edward Hosea alisema dhana ya usuluhishi ni rahisi kutekelezeka kama mawakili wa kujitegemea watabadili fikra.



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na Jaji Mkuu, Ibrahim Hamis Juma (wa pili kulia), baada ya Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Sheria Tanzania kwenye viwanja vya Chinangali, jijini Dodoma jana. Kulia ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson. **PICHA: IKULU**





# RITA yaelimisha umuhimu kuasili mtoto kisheria

**Na Asha Bani,** DODOMA

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umeelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuasili mtoto kisheria ili kumwezesha kupata mahitaji ya msingi katika jamii.

Ofisa Sheria kutoka RITA, Emmanuella Mwingira, akizungumza katika wiki ya sheria iliyofanyika jijini hapo, alisema, watu wengi hawafahamu umuhimu wa kufuata hatua za kisheria ili kuasili mtoto, katika maadhimisho hayo wanatoa elimu hiyo kwa kina ili kuondoa sintofahamu hiyo katika jamii.

"Inafahamika kuwa katika jamii yetu ya kitanzania wapo watoto wanaokulia katika vituo vya kulelea watoto yatima ama kwasababu ya wazazi kufariki, hawajulikani walipo au hawana uwezo wa kuwapatia matunzo vivyo hivyo wapo watu wazima ambao wanashauku ya kuwa na mtoto hata wa kuasili na hiyo ni kwasababu ya pengine kutojaaliwa kuwa na watoto wa kuwazaa, lakini pamoja na hayo ni muhimu kufuata sheria ili kuasili mtoto rasmi," alisema Emmanuella.

Alisema jumla ya vyeti 975 vimesajiliwa na RITA kutokana na watu mbalimbali kuleta maombi yao ya kutaka kusajili cheti cha kuasili mtoto na kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 imeweka utaratibu wa kusaidia watu wenye uhitaji.

"Kuasili mtoto kisheria ili kupata matunzo ya kudumu ya kifamilia ambapo suala hilo linasimamiwa na sheria ya kuasili Sura ya 335 toleo la mwaka 2002."

"Hata hivyo ili kusajili cheti cha kuasili mtoto kisheria katika ofisi za RITA mwombaji anapaswa kuwasilisha nakala ya uamuzi kutoka Mahakama Kuu na pia cheti cha kuzaliwa cha mtoto anayeasiliwa ili kumwezesha kupata mahitaji yake ya msingi kama elimu, chakula, malazi na masuala ya afya kwa ujumla kama watoto wengine wanavyopata katika jamii." Alisema moja ya haki za mtoto ni kulindwa jambo ambalo watoto wasiokuwa na wazazi wamekuwa wakiteseka kwa kuishi mazingira ambayo sio rafiki, hayana ulinzi na kusababisha kufanyiwa vitendo viovu na watu wasiokuwa na maadili kama kubakwa, kunyanyaswa kijinsia.

Alisema iwapo mtu atasajili cheti cha kuasili sheria itamchukulia kuwa ni sawa na mzazi halisi wa mtoto husika hivyo itasaidia pia kupunguza wimbi la watoto wa mitaani linalokuwa kila kukicha.

"Hii itasaidia pia kwa serikali kupata takwimu sahihi ya wananchi wake katika kupanga mipango mbalimbali ya kimaendeleo katika jamii kama elimu."

RITA pia inatoa huduma ya msaada wa kisheria kuhusu usimamizi wa mirathi, kuandika na kuhifadhi wosia, elimu ya ufilisi, ndoa, talaka, usajili wa cheti cha kuzaliwa pamoja na maelezo ya kina kwa bodi za wadhamini wa taasisi kuhusu namna ya kuhuisha katiba zao.

# Samia azindua tume kuboresha utoaji haki

Na Francisca Emmanuel

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza taasisi za haki jinai zitekeleze wajibu wao kwa kuzingatia misingi ya sheria, weledi, usawa, uadilifu na mila na desturi zetu.

Alisema hayo Ikulu ya Chamwino jana wakati akizindua Tume ya kuangalia namna ya kuimarisha taasisi za haki jinai na akasema hapa duniani hakuna kitu kibaya kama kuchepusha haki ya mtu.

Rais Samia alisema tume hiyo imeundwa kutokana na kuvurugika kwa mifumo ya haki jinai kunakochangiwa na kupuuzwa kwa mifumo ya maadili hivyo kusababisha baadhi ya wananchi wasio na uwezo kupoteza haki zao.

Taasisi zitakazofanyiwa tathmini na tume hiyo ni Jeshi la Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Jeshi la Magereza na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Rais Samia alisema tume hiyo itakayofanya kazi kwa miezi minne kuanzia leo hadi Mei 30 mwaka huu, itapitia upya mifumo iliyopo nchini na kuona wapi kuna upungufu ili kuboresha utoaji haki.

Rais Samia alisema aliwachagua mainspekta wa zamani wa Jeshi la Polisi, Said Mwema na Ernest Mangu kwa kuwa waliwahi kufanya kazi kwenye taasisi hiyo na mara kadhaa kulitokea changamoto.

"Profesa Edward Hosea wewe uliwahi kuwa mtu mkubwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), na pia ulikuwa na hadhi kubwa Afrika naamini utakwenda kutusaidia, nimewateua IJP wawili wote wakati wa uongozi wao kulikuwa na changamoto mbalimbali wanafahamu," alisema.

Alisema kati ya watu 100 watakaohojiwa kuhusu haki jinai, 70 watanyoosha kidole na kuitaja polisi.

"Mimi naogopa kwenda polisi na mahakama kama sio kikazi, yaani ukiniambia niende polisi hata kama kweli nimekosewa siwezi kushtaki polisi kwa sababu naogopa kugeuziwa kesi, hata tangia mdogo naogopa haya maeneo, lakini tuangalie ni mahusiano gani yaliyopo kati ya vyombo vyetu na wananchi," alisema Rais Samia.

Alisema pia wanapaswa kuangalia utendaji wa Jeshi la Magereza kama wanafanya kazi kwa mujibu wa matakwa au wanatekeleza miradi.

### Ofisi ya Taifa ya Mashitaka

Rais Samia aliagiza ifanywe tathmini kuhusu utendaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashitaka kwa kuwa ni eneo ambalo linahusika na uandaaji wa mashitaka na kuyapeleka mahakamani.

Alisema miaka ya karibuni kulikuwa na sintofahamu wakati wa ukusanyaji wa fedha kutoka kwa watuhumiwa walioingia makubaliano na serikali ya kurudisha hasara waliyosababisha.



Rais Samia alisema kuna fedha ambazo zimekusanywa na nyingine hazijulikani zilipo na kwamba wanapofuatilia wamebaini kuna akaunti imefunguliwa nchini China.

Alisema anaamini Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk Elieza Feleshi amepitia kwenye ofisi hiyo hivyo watakwenda kubaini upungufu na mapendekezo yao katika kuboresha taasisi hizo za haki jinai.

### Mahakama

Rais alisema mahakama ilikuwa na rushwa iliyokithiri lakini kutokana na hatua walizochukua sasa hali hiyo imepungua.

"Mwenyekiti wa tume hii, Jaji Othman Chande pamoja na AG nyote mliwahi kupita kwenye mhimili wa mahakama naomba mlete mapendekezo yenu," alisema.

### Takukuru

Kwa mujibu wa Rais Samia, tume hiyo pia ina wajibu wa kuichunguza Takukuru kama watu wake wanazuia rushwa.

"Mkaangalie hawa watu wanazuia au wanahamasisha rushwa, je, ndani kusafi kiasi gani kwa sababu kubadilisha mkuu wa taasisi hakusaidii kwa kuwa anakuta mizizi pale, hivyo watamdanganya wafanye wanavyotaka lakini kumtoa anayechukua rushwa na kumuingiza asiyechukua rushwa hilo ni jambo zuri," alisema.

### DCEA

Rais ameitaja Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Dawa za Kulevya, kwamba wapo vijana wanaotegeshea watu dawa za kulevya, kuwafanyia upekuzi na kudai wamekamatwa na dawa.

Alisema jambo hilo husababisha kutia hatiani watu wasiostahili kutiwa hatiani, hivyo wahakikishe wanasimamia haki.

"Katika karne ya 21 mtu akikamatwa na kutakiwa kutoa maelezo polisi basi maelezo yake yasomeke hadi kwa DPP ili polisi asipate muda wa kubadili maelezo hayo, na ndio maana utaona watuhumiwa wanalazimishwa kusaini maelezo sio yao pembeni kuna vifungu. Mifumo inapaswa isomane tuweze kulinda haki na tusiruhusu mikono," alisema Rais Samia.

# Rais Samia akemea uchepushaji wa haki

Na MUSSA YUSUPH, *Dodoma*

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema katika kipindi cha miongo kadhaa, mfumo wa haki jinai umevurugika kwa sababu ya kupuuzwa mifumo ya maadili ambapo amekemea vitendo vya uchepushaji haki vinavyofanywa na vyombo vinavyohusika na haki jinai.

Miongoni mwa maeneo ambayo Rais Dk. Samia ameyakemea ni uchepushaji haki unaofanywa na baadhi ya askari polisi kwa raia, vitendo visivyokuwa vya kimaadili ndani ya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP), ubambikizaji kesi za dawa za kulevya, mwenendo wa magereza na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Akizungumza Ikulu ya Chamwino nje kidogo ya Jiji la Dodoma, jana wakati akizindua tume ya kuangalia namna ya kuboresha taasisi za haki jinai nchini, Rais Dk. Samia alisema wasiokuwa na uwezo wa mamlaka na kifedha, wamekuwa wakipoteza haki huku wale wanaofanya makosa vyombo husika vimekuwa vikiwaacha.

"Hakuna kitu kibaya duniani kama kuchepusha haki ya mtu, lazima tutengeneze mfumo ambao kwa kiasi kikubwa utalinda haki za watu, tukaangalie tumetetereka wapi, mapungufu yapo wapi ili tuweze kulinda haki za watu," alisisitiza.

### RUNGU OFISI YA DPP

Rais Dk. Samia alisema miongoni mwa taasisi ambayo tume inapaswa kuangalia ni namna ya uendeshaji wa ofisi ya DPP ambayo miaka kadhaa iliyopita ilikuwa ikilalamikiwa hususan utaratibu wa makubaliano na washitakiwa (plea bargain).

"Nakumbuka hapo nyuma ofisi ya taifa ya mashtaka kulikuwa kuna ngoma kubwa inachezwa mpaka kukusanya fedha za wale Plea bargain, pesa zile za Plea bargain zimeonekana, zingene hazionekani.

"Ukifuatilia utaambiwa kuna akaunti China sijui imepeleka pesa zipi. Tukatizame haya yote Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuna nini kimeharibu," alisisitiza Rais Dk. Samia.

### JESHI LA POLISI

Kwa upande wa Jeshi la Polisi, Rais Dk. Samia alisema jeshi hilo nalo linapaswa kuangaliwa kwa sababu ya uwepo wa malalamiko mengi kutoka kwa raia.

"Tukaliangalie Jeshi la Polisi ambalo kama utazungumza na watu 100, basi 70 watalalamikia Polisi. Inatakiwa mtu akikamatwa, akitoa maelezo yake yamfikie mpaka DDP aweze kuyasoma, polisi asipate muda wa kubadilisha.

Aliongeza kuwa: "Lakini namna mtu anapotoa maelezo yake ndio yenyewe au polisi anaweka yakwake?, anaandika ya kwake kisha anawekewa kirungui saini hapa. Na hayo ndiyo yanayokwenda.

"Anatakiwa mtu akisema, DDP ajue amesema kitu gani. Mifumo isomane, ndio tunavyoweza kulinda haki za watu, lakini tukiwapa watu nafasi ya kuweka mikono siku zote hatutakwenda na haki za watu," alieleza.

### UTENDAJI TAKUKURU

Katika hotuba yake, Rais Dk. Samia alisema TAKUKURU nako kunapaswa kumulikwa kama wanatekeleza majukumu yao ipasavyo au wanakuwa sehemu ya kuhamasisha vitendo vya rushwa nchini.

Alisema hata kama mkuu wa taasisi hiyo akibadilishwa endapo kukiwepo watu waliokita mizizi ndani ya chombo hicho, ni rahisi kumpotosha kiongozi ili waweze kufanya vile wanavyotaka.

"Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na yenyewe kuna nini humo ndani, je watu wanazuia na kupambana na hiyo rushwa au saa nyingine wanaihamasisha hiyo rushwa, humo ndani kupo safi kiasi gani?.

"Twendeni tukatizame kwa sababu kubadilisha mkuu wa taasisi hakusaidii, mkuu wa taasisi akiingia atakuta mizizi imeota pale ya miaka na miaka, huyu mpya watamdanganya wafanye wanavyotaka. Twendeni tukayaangalie," alieleza.

### MAGEREZA

Akizungumzia mwenendo wa Jeshi la Magereza, alisema jeshi hilo linapaswa kutizamwa kama lina hitaji maboresho ya aina gani kuendana na mahitaji ya karne ya sasa.

"Jeshi la Magereza tukatizame hali ikoje, kunahitaji maboresho ya aina gani katika karne hii ya 21, magereza yatu yapoje, yanapaswa yaweje, mwendelezo wa magereza upoje, je wanashughulika na kazi za msingi au wamejikita katika miradi zaidi," alihoji.

Kwa upande wa Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Dawa za Kulevya (DAECA), alisema kumekuwepo malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu kubambikiziwa dawa hizo.

Alisema baadhi ya watumishi wa mamlaka hiyo wanadaiwa kuwategeshea watu dawa hizo kisha baadae kuja kudai kutaka kukagua na kusema wamekata dawa za kulevya kitendo ambacho ni uchepushaji wa haki za watu.

"Tumekuwa zaidi tukijitazama sisi kuliko kutizama wengine kwa sababu unapompokonya mtu haki yake na kumpa mwingine huko ni kujitizama wewe, twendeni tukaangalie nini hasa, ni mahitaji au kitu gani, uzalendo upo wapi?," alisisitiza.

Alisema yapo baadhi ya mambo muhimu yanayopaswa kutizamwa ambayo ni mafunzo, mfumo wa ajira, upandishwaji vyeo, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), utendaji kazi na mahusiano kati ya taasisi hizo na raia.

Rais Dk. Samia alisema endapo tume hiyo ikibaini umuhimu wa mabailiko ya sheria, inapaswa kutoa mapendekezo kwa kuainisha kifungu husika na namna nzuri kinavyopaswa kusomeka huku akitoa agizo kwa vyombo vya ulinzi na usalama kutoa ushirikiano kwa tum hiyo.

### MABALOZI TUMBO JOTO

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Samia alisem kwa sasa pale panapoibuka tatizo kutaundw timu maalumu ya wataalamu kuchungu kisha kutoa mapendekezo kwa serikali ambap baada ya wiki mbili kuanzia sasa, itaundwa tim maalumu kuangalia mwenendo wa sekta y mambo ya nje.

"Huu sasa ndio utakuwa mwendo wet penye tatizo popote tutaunda timu, wataalam tunao, wengi wamestaafu, lakini ni wataalam ambao tunaweza kuwatumia kujenga tena ta letu.

Alibainisha kuwa: "Nilikuwa nanong'o na katibu mkuu kiongozi, leo (jana) tunazindu tume hii, baada ya wiki mbili hadi tatu zijaz tunazindua tume itakayokwena kuangalia sek yetu ya mambo ya nje."

"Kwa wakati huu tulionao, sekta yetu y mambo ya nje ikoje, iweje, watu wetu tuliona wanasifa ya kuitwa mabalozi?, je wanafanyaka ya mabalozi," alieleza Rais Dk. Samia.

### MAKAMU WA RAIS

Kwa upande wake, Makamu wa Rais D Philip Mpango, alisema yapo manung'uniko y wananchi yanayoonyesha mfumo wa haki jin una changamoto kuanzia ukamataji, wananc kufahamu haki zao na ucheleweshaji upelelezi.

"Wananchi wanasema mengi, labda nito mfano kuna kijana Mwanza alikamatwa mwe mmoja na nusu uliopita, wazazi walihangai kumtafuta ikashindikana. Baada ya kuhangai sana nikawasiliana na uongozi wa Polisi Mk wa Mwazna na wiki iliyopita baba mzazi akasem polisi wamekuja kumueleza mtoto wake wana wakati tayari wameshatangaza msiba," alisimu Dk. Mpango

Alisema Rais Dk. Samia ametumia hekima busara kama msimamizi wa haki kwa Watanzani hivyo alimpongeza kwa kuunda tume hi kuangalia namna ambayo Watanzania watapa haki zao.

### KATIBU MKUU KIONGOZI

Awali, Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Mos Kusiluka, alisema jukumu la tume hiyo kufanya tathmini ya kina ya mfumo wa haki jin na kufanya marekebisho makubwa ili kukid matakwa ya jamii ya Watanzania.

Alisema taasisi zitakazohusika ni polisi, Of ya DPP, TAKUKURU, Jeshi la Magereza, DAECA tayari wajumbe wataifanya kazi hiyo kwa kipin cha miezi minne.

Wajumbe wa tume hiyo ni Jaji Mkuu Mstaa Mohamed Othman Chande (Mwenyekiti), D Ombeni Sefue (Makamu Mwenyekiti), Laur Ndumaro, Jaji Elieza Fereshi, Dk. Edward Hos IGP Mstaafu Balozi Ernest Mangu, Saada Ibrahi Omar Issa, Yahya Khamis Hamad, Baraka Lena IGP Mstaafu Said Mwema.



President Samia Suluhu Hassan bids farewell to, among others, Chief Justice Ibrahim Hamis Juma (3rd-R, foreground), Constitution and Legal Affairs minister Dr Damas Ndumbaro (to the CJ's right), and National Assembly Speaker Dr Tulia Ackson (R) shortly after gracing the climax of the annual Law Week commemoration at Dodoma city's Chinangali grounds yesterday. Photo: State House

**Alhamisi 02/02/2023 Uk. 01**



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma (wa tatu kulia), baada ya kuhudhuria kilele cha maadhimisho ya siku ya sheria Tanzania yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Chinangali, Jijini Dodoma jana. Kulia ni Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson. **Picha na Ikulu**

**RAI**

**Pia, Jaji Feleshi aliwataka majaji na mahakimu kuwasilisha ofisini kwake majina ya mawakili wa Serikali watakaodhoofisha jitihada za usuluhishi. Alisema ofisi yake na ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, zitaendelea kusimamia vyema kwa niaba ya Serikali matakwa ya kisheria**

aji yao na wanapofanya mawasiliano mbalimbali na taasisi za nchi yetu," alisema.

Alisema ni muhimu kuimarisha mifumo ya haki ili iweze kutatua migogoro kwa haraka inapotokea na litawavutia wafanyabiashara na wawekezaji kwa kuwa linalenga imani ya usalama wa mali zao.

Rais Samia pia ametoa wito kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wanaohusika na masuala ya kodi kushirikiana na kuzifanyia marekebisho sheria zote zenye mizunguko inayochelewesha kesi na upatikanaji wa haki.


"Ukiangalia kunapotokea uvunjifu wa amani mara nyingi haki inakuwa imepotezwa. Na haki ikipotezwa basi

"Tunafanya juhudi za upatikanaji wa haki kwa kuipitia upya mifumo iliyopo. Kama ulivyoona jana (juzi) nilizindua tume ya kuangalia mienendo ya taasisi za hakijinai".

Kwa upande wake Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma alisema faida za usuluhishi ni pamoja na kupunguza muda wa kusikiliza shauri, kuokoa fedha ambazo zingetumika kulipia gharama za kesi.

Profesa Juma alisema usuluhishi pia unasaidia kuondoa chuki kati ya pande zinazopingana kwa kuwa wote wanakuwa washindi.

Kwa upande wake rais wa chama cha wanasheria Tanganyika (TLS), Profesa Edward Hosea aliiomba Serikali ianze kuwatumia mawakili wa kujitegemea



*ESIDENT Samia*
*uhu Hassan in*
*ouvenir photo*
*members of*
*Commission*
*Accessing*
*minal Justice*
*he country at*
*mwino State*
*use in Dodoma,*
*erday. Right*
*er is former*
*ef Justice,*
*hammed Chande*
*man, who is the*
*irman of the*
*mission and his*



***MOROGORO Zone High Court Judge Gabriel Malata (left) and his colleague Justice Messe Chaba, dance alongside members of the court's choir group at the climax of Law Week in Morogoro Region, yesterday. (Photo by John Nditi)***